BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAJUMUISHO YA MJADALA WA BAJETI ZA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia kuwepo hapa tukiwa na siha na afya njema tukaweza kutekeleza majukumu yetu. Aidha, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yenu ya kuliongoza Baraza hili kwa busara, hekima na weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upekee kabisa, naomba kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa utendaji wake makini na miongozo yake ambayo inasaidia kuhakikisha taasisi zote za Serikali zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kutoa huduma bora kwa wananchi wetu. Aidha, nawapongeza wasaidizi wake wa karibu, Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdullah kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kumsaidia Mhe. Rais ili kuyafikia maendeleo tunayoyatarajia.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upekee kabisa, naomba niwashkuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa mashirikiano yao na umahiri wao mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu. Ili kuzipa uzito shukurani zangu kwao naomba uniruhusu niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo;-

1. Mhe. Abdalla Hussein Kombo — Mwenyekiti
2. Mhe. Asha Abdalla Mussa — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed — Mjumbe
4. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu — Mjumbe
5. Mhe. Miraji Khamis Mussa — Mjumbe
6. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad — Mjumbe

Aidha, napenda kuishukuru Sekreterieti ya Kamati ya Bajeti kwa kutekeleza vyema majukumu yake hatimaye kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Sekreterieti hiyo ya Kamati ya Bajeti inaundwa na makatibu wanne (4) ambao ni:

1. Ndg. Abass Vuai Moh'd — Katibu
2. Ndg. Asha Said Mohammed — Katibu
3. Ndg. Husna Rajab Othman — Katibu
4. Ndg. Shaib Fadhil Shaib — Katibu

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 101(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2020 inaelekeza Serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti kufanya majumuisho kwa kuzingatia hoja zilizoibuka wakati wa mjadala wa Bajeti za Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza matakwa ya Kanuni hiyo, Kamati ya Bajeti ilifanya kikao na baadhi ya Wizara ambazo ziliguswa

na hoja mbali mbali zilizojitokeza katika mijadala ya Bajeti za Wizara ambazo hazikupata ufafanuzi wa kutosha ili kupata fursa ya kupatiwa majibu ya Serikali kuhusiana na hoja hizo. Hivyo, hotuba hii ni matokeo ya majibu hayo ya Serikali pamoja na maoni na ushauri wa Kamati.

## UFAFANUZI WA HOJA ZILIZOJADILIWA WAKATI WA KIKAO CHA MAJUMUISHO BAINA YA SERIKALI NA KAMATI YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao cha majumuisho baina ya Kamati na Serikali, kulikuwa na jumla ya hoja ya tano (5) zilijadiliwa kutoka katika Wizara zifuatavyo:

i. Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
ii. Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale
iii. Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais
iv. Afisi ya Rais Ikulu
v. Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi
vi. Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa lengo la kurahisisha ufafanuzi wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati ya Bajeti, tumeziweka hoja hizo katika Sehemu Tatu; Sehemu ya Kwanza inahusu Hoja Zilizoibuliwa, Sehemu ya Pili inahusu Majibu ya Wizara na Sehemu ya Tatu ni Ushauri wa Kamati.

### Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara

## Maalum za SMZ

**Hoja:**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Fungu D06, Kikosi cha Valentia (KVZ) kimeidhinishiwa kutumia TZS 23.2 bilioni. Hata hivyo, hakuna taarifa ya makadirio ya mapato yatakayokusanywa na kikosi hichi. Kamati iliomba kupatiwa ufafanuzi wa makadirio hayo ya mapato kwa mwaka 2022/2023.

**Majibu ya Wizara:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kwamba, kwa sasa Kikosi cha Valentia hakifanyi makusanyo yoyote kwa sababu hakina vyanzo vya mapato na hakijishughulishi na mradi wowote. Awali kikosi hichi kilikuwa kinakusanya kupitia ada za ulinzi. Hata hivyo, kwa sasa, baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Uwakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Nam. 2, 2015, jukumu hili kisheria linatekelezwa na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU).

**Maoni ya Kamati:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na kikosi hichi kubuni miradi ambayo itakiingizia mapato kikosi hichi na hatimae kiweze kuchangia mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

**Hoja:**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Bajeti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale hakujainishwa kiasi cha fedha ambazo zitatumika kwa ajili ya

matengenezo ya Jengo la Beit al-Ajaib. Kamati iliomba kupatiwa ufafanuzi wa makadirio ya fedha ambazo zitatumika katika matengenezo hayo kwa mwaka 2022/2023.

**Majibu ya Wizara:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kwamba gharama za matengenezo ya Beit al-Ajaib ni Dola za Kimarekani milioni 25 ambazo ni sawa TZS 57.5 bilioni. Imeelezwa kwamba, fedha hizo zitagharamiwa na Serikali ya Oman.

**Maoni ya Kamati:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Wizara kuweka wazi gharama na taarifa zote za kifedha ili kuwe na urahisi wakati wa upitishwaji wa bajeti zake Barazani pamoja na kuweza kuzitumia taarifa hizo wakati wa ukaguzi wa mradi.

**Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**

**Hoja:**

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mwaka 2022/2023 imepangiwa kutumia TZS 4.9 bilioni, kiasi ambacho ni kidogo ukilinganisha na majukumu yake. Ukiangalia Fungu PB0101 la Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi ambalo limepangiwa TZS 6.25 bilioni. Kamati inashauri, fedha za Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi zipunguzwe na zikaongezwe katika bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Majibu ya Wizara:**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara iliiyomba Kamatikwamba Fungu hili libaki

kama lilivyopangwa awali kwani hata kiasi hicho kilichopangwa bado ni kidogo ukilinganisha na majukumu yanayokusudiwa kutekelezwa ya kuendeleza juhudi za kupambana na athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi kwa nia ya kuvihami visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha, fedha hizi ndizo zitakazotumika kutekeleza mpango wakuifanya Zanzibar kuwa ya Kijani na kufanya utafiti wa kina wa athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Maoni ya Kamati:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati baada ya kujadiliana na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kuona umuhimu wa kupambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi imekubaliana kwa pamoja kuwa, Fungu PB0101 la Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi lililopangiwa TZS 6.25 bilioni libaki kama lilivyo ili fedha hizo ziweze kutumika katika kutekeleza majukumu yaliyopangwa. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na changamoto ya uwezo wa kifedha kwa Serikali yetu, Kamati bado inasisitiza juu ya umuhimu wa kuongeza fedha kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika bajeti zijazo kwa kadri itakavyowezekana, kwani janga la dawa za kulevya limekuwa likiathiri nguvu kazi ya taifa na kuipa mzigo mkubwa Serikali katika kukabiliana na athari zinazotokana na madawa hayo.

**Afisi ya Rais Ikulu/ Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi**

**Hoja:**

**Mheshimiwa Spika**, Makusanyo ya mapato ya Afisi ya Nyaraka ambayo ipo chini ya Afisi ya Rais Ikulu kukusanywa na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Kitengo cha Utafiti. Kamati ilihoji sababu za mapato haya kutokukusanywa na taasisi husika ili kukapatikana uwazi na namna bora ya kuyaripoti mapato hayo.

**Majibu ya Wizara:**

**Mheshimiwa Spika**, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais haihusiki na ukusanyaji wa mapato ya aina yeyote yanayotokana na shughuli za utafiti hapa nchini. Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Idara yake ya Uratibu wa Shughuli za Serikali inaratibu upatikanaji wa vibali kwa wageni na wenyeji wanaoomba kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Kwa upande wake, Afisi ya Rais Ikulu kupitia Afisi ya Nyaraka inapata mapato kutokana na huduma ya utoaji wa kopi. Kiuhalisia chanzo hichi sio sahihi cha kuripotia mapato.

**Maoni ya Kamati:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Afisi ya Rais Ikulu kwa kushirikiana na taasisi husika, kuandaa muongozo juu ya ada na tozo katika huduma zote zinazotolewa na Afisi ya Nyaraka.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

**Hoja:**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji ulipaswa uwe umeshamaliza tokea Aprili 2022 lakini katika Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023, mradi umetengewa tena jumla ya

TZS 20.5 bilioni kwa ajili ya kuuendeleza ili kutekeleza shabaha tano (5). Kamati inaomba uchambuzi wa namna zitakavyopatikana fedha hizi na namna zitakavyotumika kwa kila shabaha au shughuli iliyopangwa.

**Majibu ya Wizara:**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji ambapo jumla ya fedha zilizotengwa ni TZS 20.5 bilioni ambazo TZS 20 bilioni ni mkopo kutoka Exim Benki ya Korea na TZS 500 milioni ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. **Mheshimiwa Spika**, Jumla ya TZS 15 bilioni zitatumika kwa ajili ya kuendeleza misingi ya umwagiliaji maji yenye urefu wa kilomita 26.65, misingi ya kutolea maji ya ziada yenye urefu wa kilomita 24.6, barabara za mashambani zenye urefu wa kilomita 6.9 na uchimbaji wa visima 15 vya umwagiliaji. **Mheshimiwa Spika**, Jumla ya TZS 5 bilioni zitatumika kwa ujenzi wa misingi ya ndani kwa kiwango cha saruji yenye urefu wa kilomita 47.74 katika mabonde ya Cheju A, Kinyasini, Kilombero, Kibokwa, Chaani, Cheju na Mlemele.

Jumla ya TZS 300 milioni zitatumika kwa ajili ya uungaji wa umeme wa njia kuu kwa visima 15 katika bonde la Cheju B pamoja na kumalizia uungaji wa umeme katika bonde la Kilombero na Kibokwa.

**Mheshimiwa Spika**, Jumla ya TZS 200 milioni zimetengwa kwa ajili ya kufanya malipo ya fidia kwa wananchi watakaoathirika wakati wa utekelezaji wa mradi.

**Maoni ya Kamati:**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Kamati imebaini changamoto mbali mbali katika utekelezaji wa mradi huu wa umwagiliaji kwa kipindi kilichopita ikiwemo kujengwa kwa miundombinu chini ya kiwango na fedha kutumika nje ya mkataba, Katika utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Kamati inasisitiza juu ya kufuatwa kwa taratibu zote za kisheria. Aidha, Wizara iongeze umakini katika utekelezaji wa mradi huu ili uweze kumalizika kwa wakati uliopangwa pamoja na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## MAENEO YALIYOCHANGIWA NA WAJUMBE WENGI

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa mjadala wa bajeti, baadhi ya maeneo yalichangiwa na Wajumbe wengi zaidi na baadhi ya maeneo hayo yalichangiwa kwa hisia kubwa. Michango hiyo ililenga kuisisitiza Serikali na kuitaka kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na miongozo mbali mbali ya nchi. Kwa lengo la kuikumbusha Serikali ili kuichukulia michango hii kwa uzito maalum, kwa mantiki hiyo, Kamati inayasisitizia tena maeneo haya kama ifutavyo:

### Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi

**Mheshimiwa Spika,** Suala la upatikanaji wa bajeti kwa ajili ya ununuzi wa gari zitakazotumika kuhudumia Kamati za Baraza la Wawakilishi ni jambo lililosisitizwa sana na Wajumbe pamoja na Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Ifahamike kuwa, usafiri wa Kamati ni nyenzo muhimu katika kufanikisha majukumu ya Kamati na inakuwa si busara wakati Kamati zinapotekeleza majukumu yake, kuomba usafiri kwa taasisi ambazo zinaenda kuzisimamia. Hivyo, ni

vyema tatizo la usafiri kwa Kamati za Baraza likapatiwa suluhisho ili ziweze kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo kwa maendeleo ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa maeneo yaliyozungumzwa na Wajumbe ni pamoja na kuimarishwa kwa maslahi ya watumishi wa Baraza ikiwemo mishahara na maposho ili yaende sambamba na unyeti na ugumu wa shughuli wanazozitekeleza. Kamati inaunga mkono hoja hii, kwa kuwa kuimarisha maslahi yao kutapelekea watendaji hao kufanya kazi kwa utulivu na ufanisi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** Suala la utunzaji na uhifadhi wa mazingira ni jambo lililosisitizwa sana na Wajumbe wakati wa mjadala wa bajeti wa Wizara hii pamoja na kuwataka wananchi kujiepusha na vitendo vinavyopelekea uharibifu wa mazingira sambamba na uendelezaji wa maeneo yaliyoachwa ambayo awali yalitumika kwa shughuli za uchimbaji wa mchanga. **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kulizingatia jambo hili na kuchukuwa jitihada mahsusi ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza. Aidha, Kamati inasisitiza zaidi juu ya kufanya jitihada za pamoja katika kuhifadhi na kutunza mazingira yanayotuzunguka.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusiana na kuwawezesha watu wenye ulemavu, Wajumbe walipendekeza juu ya kuangaliwa kwa mahitaji yao ya msingi ikiwemo elimu na miundombinu rafiki ya kupata elimu pamoja na kuwawezesha kiuchumi. Kamati inaishauri Serikali katika

kulisimamia jambo hili, ni vyema kuangalia Sera na Sheria zinazogusa watu wenye ulemavu zinakwenda sambamba na mahitaji yao halisi pamoja na kuitaka taasisi husika kufanya usimamizi madhubuti ili kufikia malengo yaliyopangwa.

## Afisi ya Rais Ikulu

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusiana na mfumo wa ***"Sema na Rais"***, Wajumbe wengi wamesisitiza juu ya kupewa elimu kwa wananchi na makundi mbali mbali namna ya kuutumia mfumo huo kwani bado haujaeleweka vya kutosha. Kwa kuwa mfumo huu unawawezesha wananchi kutoa maoni, changamoto na kero mbali mbali zinazowakabili kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi na Serikali, Kamati inawashauri wananchi kutumia fursa hii ipasavyo ili kuweza kutatuliwa kero na changamoto zao.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la utunzaji wa nyaraka kwa mfumo wa kielektroniki pia lilichangiwa na Wajumbe wengi na walisisitiza kuwa, Afisi ya Nyaraka kuacha mfumo wa kuhifadhi nyaraka katika nakala ngumu (hardcopies) ambao umeshapitwa na wakati. Kamati inaishauri Serikali kulifanyia kazi jambo hili na kuingia katika mfumo wa kielektroniki ili nyaraka zetu ziweze kudumu kwa muda mrefu na kurahisisha upatikanaji wake kwa watumiaji.

## Wizara ya Afya

**Mheshimiwa Spika,** Michango ya Wajumbe wengi inaonesha kuwepo kwa changamoto ya Serikali kununua vifaa tiba vya kisasa mathalan X – Ray, CT Scan na MRI lakini kunakuwepo na uhaba wa wataalamu

wa kuvitumia, kuvitunza na kuvikarabati vifaa hivyo. Kamati inaishauri Serikali, kuwepo na mpango wa kuajiri na kuwapatia mafunzo wataalamu waliopo kabla ya ununuzi wa vifaa vilivyokusudiwa ili vitakapowasili tu viweze kutumika na pia wataalamu waweze kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Wajumbe walichangia kwa msisitizo ni kuwepo kwa uhaba wa madaktari, uhaba wa vifaa tiba na uhaba wa dawa katika hospitali zetu. Hofu ya kuendelea kuwepo changamoto hii imeoneshwa na Wajumbe wengi hasa katika hospitali mpya za kila Wilaya zinazojengwa. Hivyo Kamati inaungana na Wajumbe katika kusisitiza utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi ya Hospitali mpya uendane sambamba na mpango wa uajiri.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa sana katika Mkutano huu wa Bajeti ni kuongezeka kwa vifo vya mama na mtoto ambayo ni dalili ya kuzorota kwa huduma za afya ya uzazi kulikosababishwa na upungufu wa madaktari, vifaa tiba na dawa. Pia kukosekana kwa elimu ya afya ya kutosheleza. Kamati inaishauri Serikali, kuitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto hii kama vile Waheshimiwa Wajumbe walivyoshauri, pamoja na kuwepo kwa ufuatiaji baada ya vikao vya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kukosekana kwa maadili ya wafanyakazi katika sekta ya afya hususani wauguzi na wakunga kutokuwa na huduma nzuri kwa wagonjwa pia lilichangiwa kwa msisitizo mkubwa na Waheshimiwa Wajumbe. Kamati inaungana na Wajumbe na kuitaka Serikali kuwachukulia hatua za kiutumishi watendaji wote

wanaokosa nidhamu ya kazi zao.

**Mheshimiwa Spika,** Msisitizo mkubwa umewekwa pia kwa Kujengwa kituo cha daladala karibu na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wajumbe wanahisi kwamba, eneo hili si sehemu muafaka kujengwa kituo hichi kwani italeta usumbufu kwa wagonjwa waliopo katika wodi za karibu na pia eneo hilo ni karibu na barabara ambayo inapitwa na viongozi wakuu wa kitaifa mara kwa mara. Wajumbe wamependekeza, jambo hili liangaliwe na kuamuliwa upya.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto**

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa mambo yaliyozungumza kwa msisitizo na kwa hisia kubwa katika Wizara hii ni kuendelea kuwepo kwa vitendo vya udhalilishaji katika nchi yetu. Kamati inasisitiza Serikali kuendelea kuziwezesha na kuzipa uhuru zaidi Mahkama zetu ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuweza kutoa hukumu za kesi kwa wakati. Vile vile Kamati inalitaka Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa weledi, watende haki lakini bila kuwa na muhali kwa wale wote wanaofanya uhalifu.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ni kutokupatiwa Pencheni Jamii baadhi ya wazee ambao wanastahiki kutokana na hoja ya kutokuwa na vielezo vya kutosha. Kamati inaungana na Wajumbe waliochangia hoja hii kwamba Serikali itafute vielelezo mbadala ili iweze kubaini wanaostahiki kupata pencheni hii. Mathalani, kunaweza kutumika viapo vya mahkama (affidavit) kuthibitisha umri halisi wa muhusika.

## Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

**Mheshimiwa Spika,** Kuwepo kwa migogoro mingi ya ardhi ni eneo jengine ambalo limechangiwa sana na Wajumbe. Hali hii ina athari kubwa kiuchumi kwani kuna utitiri mkubwa wa kesi mahkamani ambazo zinapoteza muda mkubwa kwa wananchi kushughulikia kesi hizo, kiasi ambacho kunapelekea kukosekana kwa muda wa kufanya shughuli za kimaendeleo lakini pia inapotokezea kudhulumiwa mwenye haki kunapelekea kumrudisha nyuma kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ni kutofanyiwa kazi Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Zanzibar (Zanzibar Land Use Master Plan) ni miongoni mwa maeneo yaliyojadiliwa na wajumbe wengi. Hali hii imesababisha kuwepo uvamizi wa ardhi kama vile maeneo ya kilimo kujengwa nyumba za makaazi na pia kutokuwa na miji iliyopangika. Kutekelezwa kwa mpango huu, kungelitatua matatizo mengi ya ardhi kama vile migogoro ya ardhi na kadhaalika.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la Shirika la Nyumba kutokuwa na ufanisi katika kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba mpya kutokana na ufinyu wa bajeti nalo lilichukuwa muda mkubwa wa Wajumbe kulichangia kwa msisitizo mkubwa. Kamati inashauri Serikali, kutekeleza kwa vitendo hatua zote zilizoshauriwa ambazo zitalifanya Shirika kujiendesha kibiashara na hatimae kuweza kupata faida na kutoa gawio kwa Serikali.

## Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara hii, Wajumbe wengi wameonesha wasi wasi wao katika utekelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu

wakati bado Mpango wa Matumizi ya Bahari (Marine Spatial Plan) haujakamilika. Licha kwamba Kamati inafahamu kwamba maandalizi ya mpango huu yanaweza kwenda sambamba na utekelezaji wa baadhi ya shughuli za uchumi wa buluu lakini ipo haja kubwa ya kuharakishwa maandalizi hayo kwani kuna uwezekano wa eneo zuri kwa uwekezaji wa shughuli za uchumi wa buluu likatumika kwa kazi nyengine kutokana na kutokuwepo kwa mpango.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo limechangiwa sana na Wajumbe ni changamoto ya kilimo cha mwani kutokuleta tija kwa wakulima. Kamati inashauri Serikali kuharakisha hatua za ujenzi wa kiwanda cha mwani na kuanza kufanya kazi kwa Kampuni ya Mwani ya Zanzibar iliyoanzishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi wameonesha wasi wasi wa ufanisi katika ugawaji wa boti 577 za uvuvi zilizonunuliwa licha ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kusema imeshirikiana na Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwani kulihitaji kufanyika utafiti wa kina. Kamati inaona kwamba, utatuzi wa kukabiliana na changamoto za namna hii ni kuwepo kwa kanzi data (database) za wavuvi ambazo zinaweza kutumika kuwabaini wavuvi watakaonufaika. Kwa sasa upo uwezekano wa kuwaacha wavuvi halisi na kupatiwa zana watu ambao hawafanyi shughuli hii.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara ya Maji, Nishati na Madini jambo ambalo limechukua muda mkubwa wa Wajumbe wako kulijadili ni

ukosefu wa upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo mengi. Kamati ya Bajeti nasi tumeona tulisisitize jambo hili kwa kuliweka katika hotuba yetu kuikumbusha Serikali kwamba eneo lenye uhaba wa maji safi na salama haliwezi kuwa na maendeleo. Muda mwingi utatumika katika kutafuta maji na sio kufanya shughuli za maendeleo na vile vile kunakuwepo na maradhi ya mripuko mara mara. **Mheshimiwa Spika,** Wizara hii kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imekuwa ikitekeleza miradi mingi inayohusiana na upatikanaji wa maji lakini kumekuwa na ufanisi mdogo sana, hivyo tunashauri Serikali ije na mkakati maalum wa kulitatua jambo hili. Ifike mahali, kadhia hii ya kukosekana kwa maji ipunguwe kwa kiasi kikubwa kama si kuondoka kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi wakati walipokuwa wakichangia bajeti ya Wizara hii, walionesha kuguswa na kuwepo kwa changamoto mbali mbali katika suala la uchimbaji wa mchanga. Licha ya Serikali kutoa majibu mazuri kuhusiana na suala hili lakini inapaswa kuendelea kuratibu vyema sekta hii kwani imeajiri wananchi wengi na pia mchanga ni muhimu sana katika sekta ya ujenzi. Kwa maelezo mafupi ni kwamba, bila ya kuwepo mchanga wa kutosha, sekta ya ujenzi itazorota.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na bei ya mafuta kutokuwa tulivu (stable) katika Soko la Dunia kutokana na vita baina ya Urusi na Ukreini, Wajumbe wengi waliweka msisitizo ya kwamba Serikali iendelee kuratibu kwa ukaribu bei ya mafuta. Kamati inaunga mkono hoja ya Wajumbe kwani jambo hili ni muhimu sana, kupanda kwa bei

ya mafuta kutaathiri moja kwa moja shughuli zote za kiuchumi na kunaweza kusababisha mfumko wa bei usiodhibitika.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mkutano huu pia kulizungumzwa tatizo la Shirika la Umeme kukosa ufanisi katika utekelezaji wa kazi zao. Kamati inaishauri kuendelea kufanya utafiti wa huduma inazozitoa kwa watumiaji wa umeme ili kuweza kutoa huduma zenye kuridhisha sambamba na kuongeza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi zake. Aidha, Serikali isaidie katika ufuatiliaji wa madeni ya taasisi zake zinazodaiwa na ZECO. Vile vile Serikali, iendeleze kwa nguvu kubwa tafiti za kuvumbua vyanzo mbadala vya umeme.

## Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe walipokuwa wanachangia katika mjadala wa bajeti ya Wizara hii, walishauri posho na stahiki za Waheshimiwa Madiwani zilipwe kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali kama ilivyo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi badala ya kutegemea kutoka katika Halmashauri au Manispaa zao ambapo inapelekea ucheleweshaji wa malipo hayo na vile vile kutofautiana malipo baina ya Halmashauri au Manispaa moja na nyengine kutokana na kutofautiana katika uwezo wa kukusanya mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Mijadala ya Wajumbe imeonesha kuwa, masoko mbadala yana changamoto ya kukosekana kwa huduma ya vyoo na kutuama maji katika maeneo ya masoko. Kamati inaishauri Serikali,

kuendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizi kabla hazijaleta madhara ya kiafya. Vile vile, Serikali ihakikishe masoko ya kudumu yanayojengwa yanamalizika kwa wakati ili wafanya biashara warudishwe katika maeneo ya awali.

**Afisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara hii jambo ambalo limechukua muda mwingi wa Wajumbe kulichangia ni kuwepo kwa uchakavu na ubovu wa Mahakama za Wilaya unaosababisha kutoleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na kutenda haki kwa wananchi. Kamati inafahamu kwamba tunakabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha lakini kutokana na umuhimu wa jambo hili, Kamati inashauri Serikali iweke mkakati wa kulitekeleza hili kidogo kidogo ili shughuli nyengine zisikwame. Jambo la muhimu kuwe na muendelezo mpaka pale mahkama zote zitakapokuwa zimemaliza ukarabati au matengenezo yaliyokusudiwa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali**

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya kwamba, kila mwaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali huidhinishiwa bajeti yao, bado wajumbe wengi walichangia changamoto ya stahiki za walimu ikiwemo maposho na madeni mbali mbali kutolipwa kwa muda unaostahiki. Kamati inaitanabahisha Serikali kwamba, ili kupatikana elimu bora ni lazima kuwepo walimu mahiri wenye weledi, morali na ari ya kufanya kazi. Mambo mengine yanayofuata ili kupatikana kwa elimu bora ni matumizi ya mitaala bora na uwepo wa miundombinu bora. Hivyo,

iwapo tunataka kunyanyua sekta yetu ya elimu ni lazima tuwe na mkakati wa kuimarisha maslahi ya walimu. Ni wazi kwamba, kuwepo kwa malalamiko mengi ya stahiki za walimu ina maana kwamba lipo tatizo kubwa linalohitaji kufanyiwa kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Wajumbe walichangia kwa msisitizo ni kuwepo kwa changamoto ya uchelewaji wa malipo ya mikopo ya wanafunzi wa vyuo. Hali hii inapelekea baadhi ya vyuo vyetu hasa vya binafsi kujiendesha kwa hasara na hatimae kushindwa kulipa hata mishahara ya waalimu na wafanyakazi wengine wa vyuo hivyo. **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kulichukulia jambo hili kwa umakini na uzito mkubwa kwani lina athari kubwa lisipofanyiwa kazi kwa haraka. Mathalan, changamoto hii inaweza kupelekea vyuo vyetu kuzorota katika utoaji wa elimu na kama tunavyojua bila ya elimu bora, maendeleo huwa ni ndoto tu. Vile vile, wanafunzi wanapokosa mikopo tunakuwa tunawaweka katika hatari ya kuingia katika vishawishi ukizingatia kuwa mikopo hiyo ndiyo inayowasaidia katika kupata huduma mbali mbali.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo**

**Mheshimiwa Spika,** Suala la wizi wa mazao na mifugo lilichangiwa kwa msisitizo mkubwa na Wajumbe wa Baraza lako. Jambo hili linahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka kwani linawarudisha nyuma wananchi kiuchumi kwa kukata tamaa ya kuendelea kufanya shughuli zao za kilimo na mifugo. Hali hii ikiendelea, itaathiri uchumi wetu kwa kiasi kikubwa kwa sekta ya kilimo na ufugaji na kupelekea kukosekana kwa mchango wa sekta hizo katika Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa sana ni

kuwepo kwa vitendo vya kuendelea kukuwa kasi ya ukataji miti kunakopelekea kuathiri kwa kiasi kikubwa misitu yetu na uoto wa asili. Kamati inaishauri Serikali, licha ya kuendelea na hatua za upandaji miti ije mkakati madhubuti wa kuhakikisha nishati mbadala ya kupikia kama vile gesi na umeme inapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu. Bila ya kuwepo nishati mbadala ya kupikia ambayo wananchi wataweza kuipata, ni jambo lisilowezekana kuwazuia wasikate miti kwa ajili ya kupata kuni au kuchoma makaa.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda**

**Mheshimiwa Spika**, Katika hoja ambazo zimeibuka wakati wa mjadala ni pamoja na kuwepo kwa utofauti wa bei za bidhaa baina ya Pemba na Unguja katika suala la gharama za usafirishaji. Hali ambayo inaleta taharuki kwa wananchi wa kisiwa cha Pemba wakati wa uuzaji wa bidhaa hizo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza katika miradi ya ujenzi wa bandari ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa husika kwa urahisi na kuweza kuwaondoshea changamoto hii wananachi wa kisiwa cha Pemba, pia kuandaa mahusiano ya kibiashara kwa nchi za karibu ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa kwa gharama nafuu.

**Mheshimiwa Spika**, Pia katika mjadala huu kulijitokeza kuwepo kwa utofauti wa kasma katika baadhi ya vitabu vya hotuba na kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi hali ambayo inaleta mkanganyiko kwa wajumbe kwa kuona kwamba bajeti haina uhalisia.Kamati inaiomba Serikali wakati wa uandaaji wa bajeti ni vyema kuwa makini ili kuepusha makosa kama hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wajumbe wengi pia walitiliaa mkazo hoja ya ufinyu wa ofisi licha ya kuwa Serikali inandaa mpango wa ujenzi wa ofisi za Serikali. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali katika kupanga bajeti yake ya ujenzi wa ofisi za Serikali iweke kipaumbele kwa zile taasisi ambazo zina uhaba mkubwa zaidi. Hali hii itaweza kuimarisha mazingira ya kazi kwa haraka na kuleta ufanisi katika kazi.

### Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

**Mheshimiwa Spika**, Katika Wizara ya Utalii, wajumbe walisisitiza suala la kuitangaza Zanzibar kiutalii kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii katika kukuza uchumi wa nchi yetu, ni vyema Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuutangaza utalii kwa kuanzisha vivutio vipya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuongeza idadi ya watalii na hatimae kuongeza Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uandaaji wa bajeti ni vyema kwa baadhi ya wizara kuainisha fedha walizozitenga na kazi ambayo itakwenda kutumika fedha hizo ili kuondosha sintofahamu kwa wajumbe wanapopitia makadirio hayo. Pia Kamati inaiomba Serikali kutenga kiasi kikubwa kwa ajili ya kazi za maendeleo ili kuandaa miradi ambayo italeta tija kwa nchi yetu.

### Afisi ya Rais - Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusiana na matumizi ya Mashine za Kutolea Risiti za Kielektroniki, Wajumbe wamechangia changamoto zilizopo kwa wafanyabiashara katika kuzitumia mashine hizo ikiwemo

baadhi ya muda mashine kushindwa kutoa risiti kwa wakati pindi wateja wanapofanya manunuzi ya bidhaa pamoja na wafanyabiashara kutoandika mauzo sahihi katika risiti wanazowapatia wateja hao. Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Bodi ya Mapato Zanzibar kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizi ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusiana na uchangiaji wa gawio kwa mashirika ya Serikali, Wajumbe wamechangia juu ya baadhi ya mashirika kushindwa kuchangia gawio Serikalini na kupelekea kushuka kwa mapato ya Serikali. Kwa kuwa Serikali haiwezi kutegemea mapato ya kodi pekee katika uendeshaji wa shughuli zake, Kamati inaishauri Serikali kufanya usimamizi madhubuti wa mashirika hayo ikiwemo kufuatilia uongozi wake na kuhakikisha mashirika yanafanya kazi kwa uweledi na kuepuka vitendo vya udanganyifu, ubadhirifu na rushwa.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la fedha zinazokusanywa na Mfuko wa Barabara lilichangiwa na Wajumbe na kusisitiza juu ya upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati pindi zinapoombwa hazina. Ifahamike kuwa, mfuko huu una jukumu la kutunza na kutengeneza barabara nchini. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuupatia Mfuko huu fedha wanazoomba ili waweze kutekeleza majukumu yao. Kufanya hivyo kutapelekea kuwepo kwa mtandao mzuri wa barabara, wananchi watakuwa na uhakika wa usafiri na kusafirisha mizigo yao kwa wakati na kufanya biashara zitakazowainua kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ukusanyaji wa mapato, Wajumbe hawakuridhishwa na Bodi ya mapato Zanzibar (ZRB) katika kiwango cha ukusanyaji wake. Kwa mwaka wa 2021/2022, Bodi ilipangiwa kukusanya TZS 525.1 bilioni na makusanyo halisi mpaka kufikia mwezi wa machi ni TZS 275.17 bilioni sawa na asilimia 52. Kamati inashauri Bodi kwa mwaka wa 2022/2023 ijitahidi katika kukusanya mapato. Aidha, kwa upande wa Serikali Kamati inaishauri kupunguza misamaha ya kodi na pindi ikibidi kutolewa kwa misamaha hiyo, ifanyike kwa uwazi ili kuepusha upotevu wa mapato.

## HOJA ZA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na hoja za kibajeti ambazo Kamati ya Bajeti tumezieleza na zilizochangiwa na Wajumbe wengi ambazo tumezisisitiza katika hotuba hii, Kamati inapenda kutoa hoja za jumla katika maeneo ambayo kwa uzito wake ni muhimu kuishauri Serikali ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa maeneo ya jumla ambayo Kamati imeona ni muhimu kuyazungumzia ni ukodishwaji wa visiwa vidogo vidogo kwa wawekezaji. Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa kuwepo kwa utaratibu mzuri utakaoweza kutumika katika kuziongoza taasisi zinazohusika na ukodishwaji huo. Aidha, makubaliano na kujenga uelewa kwa wananchi waliopo katika maeneo ya ukodishwaji ni muhimu kuzingatiwa ili kuepusha kuibuka kwa migogoro baina ya wananchi na wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Mapato ya taasisi zinazokusanya mapato

hupelekwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali lakini kuna taasisi hazipewi fedha za kujiendesha hata wanapoziomba. Kamati inaona kwamba, kuwepo kwa mfumo wa mapato kwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni jambo zuri kwani inaepusha uvujaji wa mapato, lakini ili taasisi hizo ziweze kujiendesha vyema na kuweza kukusanya zaidi hakuna budi kuingiziwa fedha kwa wakati kwani kiasi cha fedha wanachokusanya wao ni kikubwa kuliko kiasi ambacho huomba kuingiziwa kwa ajili ya shughuli za kiuendeshaji.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja nyengine ambayo Kamati imeona iipe msisitizo maalum ni kuingizwa kiasi kidogo cha fedha au kukosekana kabisa kwa fedha za Matumizi Mengineyo kwa baadhi ya taasisi za Serikali. Kamati imebaini jambo hili limesababishwa na makusanyo kidogo ukilinganisha na matarajio ya makusanyo na pia kutokuzingatia vipaumbele katika matumizi tunayofanya.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ni kuchelewa kuletwa kwa bajeti za Wizara na Serikali katika ngazi ya Kamati kila mwaka. Jambo hili huathiri ufanisi wa upitishaji wa Bajeti hizo katika ngazi ya Kamati. Kamati ya Bajeti inashauri Serikali ijipange ianze mapema mchakato wa bajeti zifikishwe Barazani mapema ili kila shughuli ifanyike katika wakati muafaka.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo la mwisho ambalo Kamati ya Bajeti imeliona ilisisitize kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo ya nchi yetu ni kuwepo kwa utekelezaji mdogo au kutotekelezwa kabisa kwa miradi ya maendeleo. Hali hii ya kuwepo miradi mingi katika bajeti zetu bila ya kutekelezwa ni dalili kwamba bajeti zetu hazina

uhalisia. Tunapanga mambo mengi lakini tunatekeleza machache tena bila ya kukamilika. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwa mara nyengine tena, kupanga bajeti ambazo tutaweza kuzitekeleza kwa asilimia kubwa. Vile vile, Serikali iongeze juhudi katika usimamizi wa fedha za miradi ya maendeleo ili kuepusha fedha hizo kutumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Mawaziri wote wakati wa mijadala ya kupitisha Bajeti za Wizara zao walitoa ahadi mbali mbali ili kuwashawishi Wajumbe waidhinishe bajeti hizo. Kamati inaomba kuwanasihi Mawaziri kutimiza ahadi hizo walizozitoa kwa Wajumbe. Aidha, Mawaziri walitoa ahadi ya kupokea maoni na ushauri wote wa Kamati zinazosimamia Wizara zao, Kamati kwa mara nyengine inawanasihi Mawaziri na watendaji wa taasisi za Serikali kutekeleza ahadi hizi. Jambo hili litaipa heshma kubwa Baraza na Serikali kwani Wajumbe wametumia muda mwingi kujadili.

**Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii kuwashkuru Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wengine wa Serikali kwa kuipa mashirikiano makubwa Kamati ya Bajeti yaliyowezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia naomba niwaashukuru tena Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kuwa watulivu na kunisikiliza kwa umakini wakati nikiwasilisha Hotuba hii ya Majumuisho ya Mjadala wa Bajeti za Wizara zote kwa mwaka 2022/2023.

Ahsanteni na naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Hussein Kombo,

...................................

Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**